N09/2/ABSWA/HP2/SWA/TZ0/XX

88092389

International Baccalaureate®
Baccalauréat International
Bachillerato Internacional

**SWAHILI B – HIGHER LEVEL – PAPER 2**
**SOUAHÉLI B – NIVEAU SUPÉRIEUR – ÉPREUVE 2**
**SUAHILI B – NIVEL SUPERIOR – PRUEBA 2**

Tuesday 3 November 2009 (morning)
Mardi 3 novembre 2009 (matin)
Martes 3 de noviembre de 2009 (mañana)

1 h 30 m

---

INSTRUCTIONS TO CANDIDATES

- Do not turn over this examination paper until instructed to do so.
- Choose one task.

INSTRUCTIONS DESTINÉES AUX CANDIDATS

- Ne retournez pas cette épreuve avant d'y être autorisé(e).
- Choisissez une tâche.

INSTRUCCIONES PARA LOS ALUMNOS

- No dé la vuelta al examen hasta que se lo autoricen.
- Elija una tarea.



© International Baccalaureate Organization 2009

*Andika maneno yasiyopungua 400 juu ya* ***angalau mojawapo*** *ya haya yafuatayo.*

**1.** Hivi karibuni ulikuwa na fursa ya kuhudhuria maonyesho ya shule yako kwa umma kuhusu maendeleo yake na mchango wake kwa ujenzi wa taifa. Rafiki yako kutoka nchi ya ng'ambo amesikia kuhusu maendeleo ya shule yako na mchango wake kwa ujenzi wa taifa and angependa kuitembelea shule yako. Mwandikie barua ukimwalika kwa shule yako. Katika barua mweleze maendeleo ya shule yako na mchango wake kwa ujenzi wa taifa (kuandaa viongozi wa kitaifa katika siasa, udaktari, uhandisi…).

**2.** Serikali yako imeanzisha kampeni kabambe za kuwafunza wakulima nchini njia mbalimbali ambazo wanaweza kutumia teknolojia kuyaongeza mazao yao na kuyapanua masoko yao. Wewe ukiwa msimamizi wa klabu cha kilimo shuleni mwako umeombwa kuandika kijitabu kidogo kitakachopeanwa kwa wakulima wakati wa mkutano wao wa kila mwaka. Kijitabu kinastahili kueleza njia mbalimbali ambazo wakulima wanaweza kutumia teknolojia kuongeza na kuyauza mazao yao.

**3.** Shule yako imepata ombi kutoka kwa shule mojawapo maskini nchini mwako ambayo ingependa kupata msaada wa kifedha na vifaa vya kuboresha majengo, maktaba na michezo. Wewe ukiwa mwanachama wa klabu cha mipango ya kijamii umeombwa kuwahutubia wanafunzi shuleni mwako juu ya njia mbalimbali ambazo wanaweza kuzitumia kuisaidia shule hii. Andika hotuba yako.

**4.** Hivi karibuni kumekuwa na malalamiko mengi katika jamii yako kuhusu ongezeko la taka mitaani jambo ambalo linahofiwa kuihatarisha afya ya jamii. Wewe ukiwa mwanachama wa chama cha mazingira shuleni mwako umeombwa na gazeti la shule kuandika makala kuhusu njia mbalimbali ambazo shule na wanafunzi wanaweza kutumia kuiweka shule, vifaa vya shule, na mazingira ya shule na jiji safi. Katika makala eleza madhara yatakayotukia kama mazingira hayatawekwa kwenye hali safi.

**5.** Ubora wa shairi hutegemea dhamira yake na jinsi ambavyo mshairi ameyajenga maudhui yake. Huku ukitoa mifano kutoka kwa mojawapo wa shairi ambalo umelisoma darasani jadili kauli hii. Unaweza kutumia mifano ya mashairi kutoka kwa lugha yoyote.

**6.** Shule yako ingependa kuchagua kiranja mkuu ambaye atasimamia shule yako mwaka ujao. Wewe ukiwa mmojawapo wa kamati inayosimamia uteuzi huu umeombwa na mwalimu mkuu kuyakusanya mapendekezo ya wanafunzi kuhusu sifa ambazo zinaweza kutumiwa kumchagua kiranja bora. Andika ripoti ya mapendekezo ya wanafunzi.